# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU

***Dar es Salaam***
***05 Julai, 2025***

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ametoa wito kwa viongozi wa dini kuendelea kuimarisha maadili ya jamii kupitia mafundisho yanayojenga hofu ya Mungu, hususan katika kipindi hiki ambacho maendeleo ya TEHAMA yameongeza kasi ya mabadiliko ndani ya jamii.

Rais Dkt. Samia ametoa wito huo leo mara baada ya kuzindua hema la ibada la Kanisa la Calvary Assemblies of God (Arise and Shine) lililopo Kawe, linaloongozwa na Mtumishi wa Mungu Mtume Boniphace Mwamposa.

Rais Dkt. Samia amesema jamii inapaswa kuchukua tahadhari ya matumizi ya teknolojia ili kunufaika na faida zake bila kuathiri maadili, huku akiwataka viongozi wa dini kutumia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii kueneza mafundisho kwa waumini na jamii kwa ujumla.

Aidha, Rais Dkt. Samia amesifu mchango wa taasisi za kidini katika kukuza maadili, mshikamano, pamoja na maendeleo ya kiroho, kiuchumi na kijamii, na kutoa pongezi kwa taasisi hizo kwa mchango wao katika kushughulikia changamoto za kijamii na kutoa huduma mbalimbali kwa wananchi.

Halikadhalika, ameeleza kuwa Serikali inatambua na kuthamini mchango mkubwa wa taasisi hizo katika kujenga jamii yenye maadili, mshikamano na maendeleo endelevu.

Vilevile, Rais Dkt. Samia amebainisha kuwa Serikali itaendelea kushirikiana kwa karibu na taasisi za kidini, ikiwemo kuweka mazingira wezeshi ya kutekeleza shughuli zao kwa manufaa ya Taifa, pamoja na kutoa misamaha ya kodi kwa huduma zisizolenga kupata faida.

Rais Dkt. Samia amewahimiza Watanzania wote kuendelea kuliombea Taifa kwa imani tofauti ili liendelee kudumu katika amani, mshikamano na utulivu.

Shaaban Kissu
Naibu Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu